# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE MKUTANO WA MAWAZIRI WA SEKTA YA KAZI NA AJIRA NA WADAU WA UTATU WA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA (SADC) ULIOFANYIKA TAREHE 05 MACHI, 2020 KATIKA UKUMBI WA KIMATAIFA WA MWALIMU JULIUS NYERERE - DAR ES SALAAM

*Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;*

*Mheshimiwa Mouldine Castico, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*

*Dr. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika;*

*Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta ya Kazi na Ajira kutoka nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC);*

*Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi;*

*Makatibu Wakuu;*

*Ndugu Wellington Chibebe, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani Kanda ya Afrika Mashariki;*

*Mwenyekiti wa Jukwaa la Vyama vya Waajiri Kusini mwa Afrika (SPSF);*

*Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi la Kusini mwa Afrika (SATUC);*

*Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa;*

*Ndugu Wananchi mliojumuika pamoja nasi;*

*Mabibi na Mabwana;*
*Habari za Asubuhi!*

**Salaamu na Shukrani**

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutujalia afya njema na kutukutanisha hapa katika tukio hili muhimu. Pili, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania napenda kuchukua fursa hii kukukaribisheni hapa Tanzania na hasa katika Jijini letu la Dar es Salaam, ambapo Mkutano huu wa Mawaziri wa Kazi na Ajira na Wadau wa Utatu unafanyika. Aidha, kwa dhati kabisa napenda kukupongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi na Ajira kwa kunialika kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Mkutano huu muhimu kwa wafanyakazi na waajiri kutoka katika Jumuiya yetu ya SADC. Naomba niwahakikishie kwamba Dar es Salaam ni sehemu tulivu yenye amani na usalama na sina shaka yoyote kuwa mtafurahia hali hii kwa muda wote mtakaokuwa hapa.

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Napenda pia nichukue nafasi hii kuishukuru Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika pamoja na wote walioshiriki kuandaa Mkutano huu unaokutanisha Mawaziri, Makatibu Wakuu, Watendaji Wakuu na Maafisa wa Serikali pamoja na Wadau wa Utatu kutoka nchi 16 za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika hapa Tanzania. **Kwa wageni wetu, *Karibuni sana Tanzania, Karibuni nchi ya Kilimanjaro, Serengeti na Fukwe za kuvutia za Visiwa vya Zanzibar.***

**Kauli Mbiu ya Mkutano**

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Mkutano huu unafanyika kukiwa na Kauli mbiu inayosema "***Kukuza soko la Ajira na Mahusiano Mazuri Sehemu za Kazi kwa Maendeleo Endelevu***".

Mtakumbuka kwamba Kaulimbiu hii ilipitishwa katika Mkutano wa Mawaziri uliofanyika mwezi Machi, 2019 Jijini Windhoek, Namibia kwa lengo la kutukumbusha jukumu letu la msingi la kuweka mikakati mahususi ya kuongeza fursa za ajira yenye staha pamoja na mikakati ya kuimarisha mahusiano mazuri kati ya waajiri na wafanyakazi katika sehemu za kazi, na hatimaye kuchochea maendeleo endelevu ya kiuchumi katika Jumuiya yetu.

Ni matumaini yangu kwamba yale yote mtakayoyajadili na kukubaliana katika Mkutano huu mtayaelekeza katika kuweka Mikakati ya kuboresha sekta ya Kazi na Ajira kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika sekta na pia kufanikisha utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) hususan lengo namba 8 linalohimiza kuongeza fursa za ajira zenye staha (Decent Employment Opportunities Creation).

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Napenda kuwapa taarifu kuwa tarehe 14 Septemba, 2019 Tanzania iliungana na nchi nyingine wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) kusherehekea maadhimisho ya miaka 100 tangu kuanzishwa kwa Shirika hilo. Sambamba na maadhimisho hayo, Tanzania ilipata fursa ya kuzindua Mpango wa Kitaifa wa Mafunzo ya Kukuza Ujuzi wa Vijana kama sehemu ya utekelezaji wa Ripoti ya Tume ya Kimataifa kuhusu Mwelekeo wa Masuala ya Kazi kwa Nyakati Zijazo *(The Global Commision Report on Future of Work)* ambayo imesisitiza kuongeza uwekezaji katika ujuzi wa nguvu kazi hususan ya vijana. Nimeona katika ratiba ya Mkutano wenu huu kuwa mtapata fursa ya kuzindua sehemu ya vipengele vya Mkakati huo ambayo ni mafunzo ya uzoefu kazini (*internship training*).

Maadhimisho ya miaka mia moja tangu kuanzishwa kwa Shirika la Kazi Duniani (ILO) yamefungua ukurasa mpya wa kimtazamo kuhusu namna ya kuibua fursa za ajira zenye kuzingatia na kutoa haki za kijamii kwa kushirikisha wadau wake muhimu ambao ni wafanyakazi na waajiri. Mtazamo huo umelenga kutatua

changamoto za uwepo wa matumizi makubwa ya teknolojia, mabadiliko ya tabia nchi, ongezeko la watu, kuongezeka kwa sekta isiyo rasmi na ongezeko la umaskini, masuala ambayo yasipofanyiwa kazi kwa umakini yana athari kubwa katika ukuzaji wa fursa za ajira zenye staha. Ni dhahiri kwamba tunahitaji kukua kwa teknolojia na matumizi yake lakini kwa kiwango kikubwa teknolojia inachukua nafasi za watu katika kufanya kazi. Teknolojia inakuwa nzuri pale inapozalisha ajira na si inapopunguza matumizi ya nguvu kazi. Hivyo, kinachohitajika ni kuhakikisha kunakuwa na *balance* kati ya matumizi ya nguvu kazi na ya teknolojia ili kuhakikisha vijana wetu wanaendelea kunufaika na fursa za ajira zinazozalishwa.

**Sera na miongozo ya sekta ya Kazi na Ajira katika Jumuiya**

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Jukumu letu la msingi kama Wadau wa Utatu ni kuweka mazingira ya kisera na miongozo itakayowezesha uhamasishaji wa Sheria na Kanuni katika nchi zetu zitakazoweka Misingi ya Haki na Usawa katika kupata fursa za ajira na kuimarisha mahusiano mema kati ya Waajiri na Wafanyakazi. Ninafahamu kuwa haki hizi zimeainishwa kwenye Mikataba ya Msingi ya Shirika la Kazi Duniani na ile ya kipaumbele kwa Jumuiya yetu. Aidha, kwa upande wa Jumuiya yetu bado hatujaweka miongozo ya kutosha kuhakikisha malengo ya Kazi zenye Staha yanafikiwa. Hivyo, ni matarajio yangu kuwa katika kikao hiki mtajadili, kukubaliana na kupendekeza miongozo bora ya kusimamia sekta ya Kazi na Ajira.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatumia fursa hii kulishukuru Shirika la Kazi Duniani kwa misaada ya kitaalamu na kifedha ambayo Shirika hilo limeendelea kuitoa kwa nchi wanachama wa SADC na kuziwezesha kuridhia baadhi ya mikataba muhimu ya Shirika la Kazi Duniani pamoja na kuzijengea uwezo katika kutekeleza matakwa ya mikataba hiyo na hata katika uwasilishaji wa ripoti stahiki. Bila shaka Sekretarieti ya SADC na Shirika la Kazi Duniani wataendelea kuhamasisha na kuwezesha nchi zetu kuridhia Mikataba ya Shirika la Kazi

Duniani ambayo Jumuiya yetu imeipa kipaumbele ili iweze kutekelezeka na hatimaye nchi zetu zifikie viwango vya kazi vya kimataifa.

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Ukosefu wa ajira kwa vijana umebaki kuwa changamoto ya Kidunia. Kwa mujibu wa Taarifa ya Shirika la Kazi Duniani kuhusu Mwenendo wa Soko la Ajira kwa mwaka 2020, zaidi ya watu milioni 187.7 (sawa na asilimia 5.4) duniani hawana kazi na takriban wafanyakazi bilioni 2 (sawa na asilimia 61.12) wanafanyakazi katika sekta isiyo rasmi. Aidha, zaidi ya watu milioni 267 (sawa na asilimia 22) wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 hawapo kwenye mafunzo wala katika ajira. Ni vijana milioni 429 (sawa na asilimia 36) tu ndiyo waliopo kwenye mafunzo, na waliopo katika ajira ni milioni 509 (sawa na asilimia 42). Hii ni changamoto kubwa ambapo sisi Jumuiya ya SADC kama sehemu ya Dunia, inatuhusu na tunalazimika kuweka mikakati ya kupambana nayo.

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Kama mnavyofahamu maendeleo ya nchi yoyote kwa kiasi kikubwa huletwa na nguvu kazi ya vijana. Kwa wastani inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 60 ya nguvu kazi katika Jumuiya yetu ni vijana. Kwa mantiki hiyo hatuna budi kuitumia nguvu kazi hii ipasavyo ikizingatiwa kuwa yapo mahusiano makubwa kati ya nguvu kazi hiyo na ukuaji wa uchumi wa nchi zetu na katika kuondoa umasikini. Ni wazi kuwa mtu akipata ajira hupunguza kiwango cha umasikini kwa njia moja au nyingine. Na kwa msingi huo, sisi kama Jumuiya hatuna budi kuwekeza katika kuwajengea vijana uwezo wa kushiriki vizuri na kwa tija katika ukuzaji wa uchumi wa nchi zetu.

**Uhamaji wa Nguvu Kazi**

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Katika dunia ya sasa kuna matumizi makubwa sana ya sayansi na teknolojia ambayo yamechukua nafasi kubwa ya matumizi ya nguvu kazi (Rasilimali watu), na hivyo kusababisha uhamaji wa nguvu kazi kutoka sehemu moja hadi nyingine kuongezeka sana. Uhamaji wa nguvukazi hiyo umekuwa na matokeo chanya na hasi katika nchi za SADC. Matokeo chanya ni pale ambapo nchi zetu zinanufaika na uendelezaji wa ujuzi wa nguvu kazi kutoka nchi za nje au nchi zilizoendelea.

Ni ukweli usiopingika kuwa maendeleo ya kiuchumi yaliyopatikana kutokana na utangamano uliopo katika ukanda wetu yamewezesha uhamaji wa nguvu kazi kutoka nchi moja kwenda nyingine, kwa ajili ya kufanya kazi katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, madini, huduma za fedha na huduma za kijamii. Hivyo, suala la uhamaji wa nguvu kazi ni suala muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi kwa nchi zetu na hatuna budi kulitengenezea mikakati mizuri itakayowezesha wananchi wetu kunufaika.

Nimejuilishwa kwamba katika ajenda za Mkutano wenu mtajadili suala la kuwezesha uhamaji nguvu kazi ndani ya Jumuiya yetu na hata nje ya Jumuiya. Hivyo, naamini kuwa kupitia Mjadala huo mtaweza kufikia maamuzi yaliyo sahihi na kuona ni kwa jinsi gani tutawezesha nguvu kazi inayohama katika ukanda wetu wa Kusini mwa Afrika kupata fursa za ajira zenye staha pamoja na kuwezesha uhamishaji wa mafao ya Hifadhi ya Jamii *(Portability of Social Security Contributions and Benefits).*

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Kama nilivyosema awali, nimetaarifiwa kwamba sambamba na mkutano huu kutakuwa na uzinduzi wa programu ya Taifa ya mafunzo ya vitendo kwa wahitimu (yaani internship training programme), mafunzo ambayo pamoja na

mambo mengine yanalenga kuwaandaa wahitimu kuweza kupata uzoefu wa kazi na ujuzi wa kuajiriwa au kujiajiri. Hii ni jitihada kubwa inayofanywa na Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Nichukue fursa hii kuwashukuru waajiri wote wanaoiunga mkono Serikali yetu katika jitihada za kutatua changamoto za ajira kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu nchini. Mara nyingi vijana wasomi wanapomaliza masomo yao hukosa ajira kutokana na kigezo cha kukosa uzoefu wa kazi, suala ambalo serikali tumeliona na tunalitafutia ufumbuzi. Niwasihi wenzetu katika nchi za SADC ambao bado hawajaanzisha utaratibu huu, wajifunze kutoka kwetu Tanzania na wakiona utaratibu huo unafaa, basi wautekeleze kwa manufaa ya vijana wa Jumuiya yetu.

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua nafasi hii tena kukuombeni Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu mliohudhuria Mkutano huu kufanya maamuzi stahiki juu ya mambo yaliyopangwa, na kwa kuzingatia majukumu yaliyokubaliwa Kikanda na Kimataifa hususan yale yanayolenga kufikia Kazi zenye Staha.

Ni wajibu wenu kama viongozi kufanya maamuzi, kuyatekeleza na kusimamia yale yote yanayoazimiwa na kutolewa maamuzi kwa kushirikiana na Wadau wetu wa Utatu. Wafanyakazi na Waajiri wana wajibu wa kushiriki katika maamuzi yanayohusu Soko la Ajira na hii ndiyo kanuni ya msingi ya Shirika la Kazi Duniani inayozungumzia ushirikishwaji wa wadau wa Utatu katika kufikia maamuzi yanayohusu Sekta ya Kazi na Ajira.

***Waheshimiwa Mawaziri na Wadau wa Utatu,***

Mniruhusu nitumie fursa hii kukumbusha kwamba tarehe 8 Machi, ya kila mwaka ni siku ya Wanawake Duniani. Vile vile, mwaka huu 2020 ni mwaka wa 25 tangu kumetolewa tamko la maamuzi ya Beijing, kuhusu haki za Wanawake (Beijing

Platform of Action). Ndani ya Sekta yetu ya Kazi na Ajira kuna mambo mengi ya kuangalia ili tuweze kupunguza udhalilishaji wa Wanawake makazini, pamoja na kuangalia usawa wa kijinsia katika sehemu za kazi.

Ni furaha na heshima kubwa kwangu kuitumia fursa hii, kwa heshima na taadhima kutamka kuwa sasa ***MKUTANO WA MAWAZIRI WA SEKTA YA KAZI NA AJIRA NA WADAU WA UTATU WA NCHI WANACHAMA WA JUMUIYA YA MAENDELEO KUSINI MWA AFRIKA (SADC)*** umefunguliwa rasmi.

Ninawatakia Mkutano mwema.

**Mungu Ibariki Jumuiya yetu ya SADC**
**Mungu Ibariki Tanzania**
**Mungu Ibariki Afrika**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**